THE UNION FOR MULTI – PARTY DEMOCRACY
OF TANZANI

# UMD

## (KANUNI YA CHAMA)

TOLEO LA MWAKA 2000.

Toleo la Kwanza 2000

# THE UNION FOR MULTI – PARTY DEMOCRACY OF TANZANI

# UMD

## (KANUNI YA CHAMA)

TOLEO LA MWAKA 2000

Toleo la Kwanza 2000

# KANUNI ZA CHAMA.

## THE UNION FOR MULTI-PARTY DEMOCRACY OF TANZANIA(UMD)

### (1); TAFSIRI ;

Kanuni hizi zitajulikana kama **"Kanuni za UMD (The Union For Multi-Party Democracy Of Tanzania)".**

Katika kanuni hizi ila pale inapoelezwa vinginevyo au pale ambapo Tafsiri iliyopo inapingana na Katiba ya Chama, ambapo tafsiri ya maelezo ya Katiba ndio sawa mbele ya neno hilo, basi maneno yaliyoorodheshwa yatakuwa na maana kama ilivyoelezwa:-

"**Chama**" Maana yake ni 'The Union For Multi Party Democracy of Tanzania UMD.'

"**Chama cha Siasa**" maana yake ni chama cha ndani ya nchi na nchi za Nje ambacho kinatambuliwa kwa mujibu wa sheria a nchi husika kufanya shughuli za kisiasa.

"**Katiba**" maana yake ni katiba ya Chama.

"**Katibu Mkuu**" maana yake ni Katibu Mkuu wa Chama hiki.

"**Kikao cha Chama**" maana yake ni Kikao chochote cha chama katika ngazi yoyote ambacho ni halali kwa mujibu wa katiba hii.

"**Kitengo**" maana yake ni idara ya chama katika ngazi yoyote kinachoshughulikia dhamana iliyoainishwa.

"**Mtumishi**" maana yake ni Mwanachama au mtu yoyote ambaye amepewa dhamana fulani katika afisi za chama hata kama halipwi kutokana na dhamana hiyo.

## (2) UANACHAMA

1. Uanachama utakuwa wa mtu mmoja mmoja binafsi.

2. Raia yoyote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi na mwenye akili timamu ambaye ameikubali Katiba ya chama hiki, akiomba kuwa Mwanachama na pindi akikubaliwa, atakuwa ni Mwanachama wa Chama hiki. Mtu aliyekubaliwa kuwa Mwanachama atalipa kiingilio na ada ya kila mwezi kama zitakavyopangwa na Mkutano Mkuu wa chama.

3. Mwanachama anaweza kujilipia ada yake kwa jumla kila Mwaka au Mwezi hadi Mwezi.

4. Mwanachama atakabidhiwa kadi yake na Mwenyekiti wa Tawi au na Kiongozi mwingine yoyote wa ngazi ya juu. Tawi pia likipenda linaweza kufanya sherehe maalum ya kukabidhi kadi kwa wanachama walio zaidi ya mmoja.

5. Mwanachama atakuwa na haki zote za Chama na anaweza kuchagua na/au kuchaguliwa kwa mujibu wa Katiba, utaratibu na kanuni zilivyo.

6. Mwanachama anaweza akipenda kutoa Ruzuku, msaada au kuchangia kitu chenye manufaa katika ngazi yoyote ya Chama mradi tu Ruzuku hiyo au Msaada huo au Mchango huo ni halali na unakubalika.

7. Mwanachama anapotoa ruzuku hiyo au Msaada huo atakabidhi kwa Katibu wa ngazi inayohusika na atapewa risiti. Endapo ataacha Chama Ruzuku na misaada aliyotoa hatarejeshewa.

## (3) NIDHAMU YA CHAMA:

1. Kwa madhumuni ya kuhakikisha Nidhamu ya Chama bila ya kuathiri Sheria za Nchi, kila mwanachama atazingatia kwa ukamilifu misingi ya Nidhamu kwa mujibu wa Katiba ya Chama.

2. Endapo utatokea mgongano wa Wanachama kwa wanachama utadhibitiwa na kanuni za chama kwa mujibu wa uzito wa kosa lilivyo katika ngazi za chama zinazohusika na kwa mujibu wa utaratibu wa chama ulivyowekwa,

3. Ikiwa Mwanachama hakuridhika na uamuzi wa ngazi yake ana haki ya kuomba rufaa katika ngazi ya juu mpaka Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama. Ukataji rufaa utategemea na matakwa ya Katiba.

4. Mwanachama atakaepoteza sifa za uanachama atarudisha kadi yake ya uanachama katika Tawi lake la zamani ambalo alichukua kadi hiyo. Endapo Tawi hilo la zamani liko mbali naye basi atairudisha kadi hiyo katika Tawi lolote la UMD lililo karibu naye mradi tu, Tawi hili lihakikishe kwamba kadi hiyo inarudishwa Makao Makuu au Afisi Kuu au Ofisi ya Wilaya ya Tawi la zamani.

5. Mwanachama muadilifu atakuwa yule anayeheshimu Katiba, anayefuata Kanuni, anayelipa ada zake kwa wakati na anayehudhuria vikao vinavyomhusu.

6. Mwanachama asiyelipa ada zake kwa muda wa miezi 12 (Mwaka mmoja), au asiyehudhuria vikao vya chama vinavyomhusu kwa vikao zaidi ya vitatu mfululizo bila udhuru atakuwa amejiachisha mwenyewe uanachama na amepoteza wadhifa wake.

7. Mwanachama yoyote anayeshutumiwa kwa kosa lolote lile ni lazima apewe nafasi ya kujitetea katika ngazi yoyote ile anayofikishwa; na kwa vyovyote vile vyombo vinavyomtuhumu vionekane kufanya haki na visiwe na upendeleo.

UONGOZI NA MAADILI;

1. Uongozi katika UMD ni ule unaotokana na kuchaguliwa au kuteuliwa katika ngazi yoyote ya Chama uliofanywa na Mamlaka yenye uwezo huo. Uongozi huo unaweza kuwa wa muda mfupi au muda mrefu, lakini kwa vyovyote vile hautazidi miaka mitano.

2. Kwa Kiongozi wa kuchaguliwa, kila baada ya miaka mitano kiongozi huyo ataweza kuomba kuchaguliwa tena kwa nafasi anayoshikilia au nafasi nyingine.

3. Kwa Kiongozi wa kuteuliwa, Kiongozi huyo atashikilia nafasi hiyo kwa muda ambao Mamlaka iliyomteua itaainisha.

4. **Maadili ya Chama ni pamoja na :-**

   (a) Kujituma kwa hiari na kukwepa uvivu.
   (b) Kuchukia uchoyo na Khiyana.
   (c) Kujiepusha na tabia ya kusema uongo, kupika au kukaribisha Majungu na kutia au kupokea fitina,
   (d) Kujitweza na kuwa na ukiritimba wa mawazo pamoja na kutawaliwa na ubinafsi na umimi
   (e) Kukipenda Chama na Wanachama wake, kukikubali, kuilinda na kieneza Itikadi ya chama na Sera za Chama wakati wa furaha na wakati wa msiba
   (f) Kuwaheshimu viongozi wa Chama.
   (g) Kukosoa na kukubali kukosolewa kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

## HATUA ZA KUDHIBITI NA KULINDA NIDHAMU KWA VIONGOZI WA CHAMA;

1. Iwapo Kiongozi wa Chama atashindwa kutekeleza wajibu wake ataonywa na Kiongozi Mkuu wa ngazi yake au Kikao cha juu cha ngazi yake kwa **Maandishi** baada ya kupewa nafasi ya kujitetea. Taarifa ya hatua hiyo itafikishwa Ngazi ya juu ya Chama.

2. Kwa kosa la pili Kiongozi huyo atapewa **Karipio**, na kwa kosa la tatu atapewa **Karipio Kali**. Karipio na karipio kali yanatolewa kwa utaratibu ule ule wa kutolewa onyo.

3. Kwa kosa linalofuatia Kiongozi huyo ataweza kuchukuliwa moja au zaidi ya hatua zifuatazo:-

   (a) Kusimamishwa Uongozi na Kikao Chenye madaraka ya kufanya hivyo.
   (b) Kuachishwa Uongozi na Kikao chenye madaraka ya kufanya hivyo.
   (c) Kufukuzwa uongozi na Kikao chennye Madaraka ya kufanya hivyo.

4. Hatua yoyote itakayochukuliwa chini ya vijifungu (a), (b), (c), ya kifungu na 3 ni lazima taarifa yake ifikishwe katika Kikao cha ngazi ya juu.

5. Iwapo Mwenyekiti au Katibu wa ngazi inayohusika anahusika na tuhuma dhidi yake au yumo katika Mgogoro na Uongozi wa ngazi yake, Kikao kinachojadili tuhuma au mgogoro huo kitahudhuriwa na Viongozi wawili kutoka ngazi ya juu za Chama katika kushughulikia tuhuma au mgogoro huo.

6. Kiongozi au Mwanachama anayetuhumiwa kwa kosa lolote lile anan haki kuelezwa kosa analotuhumiwa nalo na kisha kupewa haki ya kujitetea mbele ya mamlaka inayotaka kutoa hukumu juu ya tuhuma hizo.

7. Mtuhumiwa ajulishwe kwa maandishi kwamba anatakiwa kufika kujitetea siku hiyo, wakati na mahala tuhuma dhidi yake zitakaposikilizwa na kutolewa maamuzi. Ushahidi wa taarifa ya

kujulishwa kwake utatunzwa na kuhifadhiwa na Katibu wa mamlaka inayohusika.

8. Endapo mtuhumiwa atapata taarifa ya kuitwa kwenda kujitetea mbele ya mamlaka inayohusika na akashimdwa kufika kwa siku, wakati na pahala alipotakiwa afike bila kutoa sababu inayoridhisha kwa maandishi, basi tuhuma dhidi yake zitasikilizwa na mamlaka inayohusika na maamuzi yatakayotolewa yatakuwa ni halali na itachukuliwa kama vile mwenyewe kahudhuria na kujieleza.

## TARATIBU ZA MCHUJO WA WAOMBAJI UONGOZI NDANI YA CHAMA NA DOLA

1. Katika Uchaguzi wa Chama na Dola wa ngazi yoyote ile kila mwanachama ana haki ya kugombea.

2. Vikao vilivyoainishwa na Katiba Vya Uchaguzi ndivyo hivyo hivyo vya kuchuja wagombea. Neno uchujaji linamaanisha pia mtu kuondoa jina lake kwa hiari yake.

3. Endapo Wagombea watakuwa wengi, Mkutano wa Uchujaji unaohusika utawasikiliza wagombea nafasi inayohusika kwa kumaanisha mgombea mmjoa kujieleza. Baada ya wagombea wote kumaliza kujieleza na kujibu masuala watakayoulizwa na wajumbe wa kikao ndipo upigaji kura utakapoanza hadi kumalizika.

4. Ikiwa kikao hicho kimefanya kazi ya uchujaji. Basi wagombea wawili watakaoongoza kwa kupata kura nyingi ndiyo watakaopelekwa katika kikao cha ngazi ya juu.

5. Kabla ya uteuzi rasmi unaofanywa na Mkutano Mkuu wa Taifa kwa mgombea Uraisi wa Jamuhuri ya Muungano au Uraisi wa Zanzibar Halmashauri kuu ya Taifa itawasilisha majina ya wagombea watatu kwa nafasi hizo mbele ya Mkutano Mkuu wa Taifa, endapo wagombea wa nafasi hizo ni wengi.

6. Endapo kikao hicho ni cha Uchaguzi wenyewe, Mgombea atakaeongoza kwa wingi wa kura ndiye atahesabiwa kuwa ameshinda. Ikiwa wanatakiwa zaidi ya mshindi mmoja basi idadi inayotakiwa ya

washindi itapatikana kutoka kwa wale wenye kura nyingi kuzidi wengine.

7. Pale ambapo anahitajika mshindi mmoja tu, basi hakuna mgombea atakaehesabika ameshinda hadi awe amepata zaidi ya asilimia hamsini (50%) ya kura zote zilizopigwa.

8. Endapo hapana mgombea aliyepata zaidi ya asilimia hamsini ya kura zote, basi wagombea wawili walioongoza watapigiwa tena kura ili kupata mshindi miongoni mwao.

9. Endapo wanahitajika zaidi ya mshindi mmoja, basi wagombea watakaoongoza kwa idadi ya kura watahesabiwa wameshinda hata kama miongoni mwao wako ambao hawakupata zaidi ya asilimia hamsini ya kura.

## UTARATIBU WA KUPIGA KURA

1. Ila pale tu ambapo Katiba imeagiza vyenginevyo, maamuzi yote ya Uchaguzi katika Chama yatatolewa kwa kupigiwa kura. Uchaguzi unamaanisha pia uchujaji wa wagombea.

2. Upigaji kura utaendeshwa kwa kufuata hatua zilizoelezwa katika kifungu cha 6 cha kanuni hizi.

3. Baada ya uchaguzi kumalizika msimamizi atasoma matokeo mbele ya wagombea na kufuatia taratibu zifuatazo:
   a) Washindi watapeana mikono na walioshindwa.
   b) Walioshindwa watatoa shukurani zao kwa wapiga kura wenzao kwa pamoja au kwa kumtumia mwenzao mmoja.
   c) Walioshinda watapeana mikono wao kwa wao halafu watapeana mikono na uongozi uliosimamia uchaguzi wote wa siku hiyo.

4. Demokrasia na Haki zitawale chaguzi zote za Chama cha UMD

5. Ulinzi mkali wa Maadili Utumike kuepuka mgawanyo kutokana na kura. Kura iwe na lengo la kudumisha umoja na sio mgawanyo.

6. Anaependa kukata rufaa anaweza kutangaza nia yake hiyo ndani ya kikao hicho. Baada ya tangazo lake atatumia Katiba na Kanuni hizi kuwasilisha rufaa yake kwa ngazi inayofuata.

## KIWANGO CHA KUHALALISHA KIKAO.

1. Kikao kitakuwa halali na maamuzi yake kuwa halali endapo zaidi ya nusu ya Wajumbe wa kikao hicho wamehudhuria au wamefikia kiwango kingine chochote kilichoelezwa ndani ya katiba kwa mambo maalum.

2. Kikao hakitaharamishwa kufanya shughuli zake kwa sababu ya kuwepo nafasi tupu yoyote miongoni mwa wa Wajumbe wa kikao hicho.

3. Hali kadhalika kuwepo kwa mtu mwingine asiye kuwa Mjumbe wa kikao hicho, hakutoharamisha kikao chenyewe, Mjadala wa kikao, na wala maamuzi ya kikao hicho, hata kama mtu asiyekuwa mjumbe wa kikao hicho atakuwa ameshiriki katika mjadala wa kikao hicho.

## UTARATIBU WA KUFIKIA MAAMUZI

1. Ila pale tu katiba inaelekeza vinginevyo, masuala yote ya kikao chochote cha Chama yatatolewa maamuzi ama kwa makubaliano ya pamoja **(Concensus)** au kwa kupigiwa kura na Wajumbe waliohudhuria kikao.

2. Pale ambapo itabidi maamuzi yafikiwe kwa kupigiwa kura basi maamuzi hayo yatafikiwa kwa wingi wa kura.

3. Mwenyekiti atakuwa na kura ya kawaida. Pale ambapo kura za wanaokubali na wale wanaokataa jambo zimefungana, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi (Casting Vote).

## MAMLAKA YA KUAJIRI NA KUTEUWA WATUMISHI WA CHAMA

1. Mamlaka ya kuajiri, kuteuwa na kupandisha cheo watumishi pamoja na kuthibitisha cheo ambacho mtumishi anapewa, yatakuwa mikononi mwa Halmashauri Kuu ya Taifa, ila tu pale ambapo katiba imeelezea vyenginevyo.

2. Ajira ya chama ni kazi ya kujitolea.

3. Kupanda daraja kutategemea kuwepo kwa nafasi wazi inayostahiki kujazwa.

4. Bila kuathiri chochote kilichomo ndani ya kifungu hichi kupandishwa kutafanyika kwa mtumishi ambaye ana elimu inayostahiki, uzoefu na uwezo wa kufanya kazi inayotakiwa.

5. Nafasi tupu ikitokea lazima itangazwe ndani ya Chama, lakini katika kujaza nafasi hiyo umbele unapewa mfanyakazi anaeongoza kwa ukubwa kazini na mwenye sifa zinazohitajika. Endapo itathibitika kwamba yule anayeongoza katika orodha ya ukubwa hatazimudu kazi au dhamana za madaraka atakayopewa, nafasi hiyo itajazwa na mtu mwingine anayeonekana anasifa zinazohitajika baada ya kusailiwa wanaostahili au walioomba.

6. Nafasi kwa ajili ya kupandishwa cheo mfanyakazi inaweza kuwepo katika hali zifuatazo:-

   a. Iwapo mwenye kushika nafasi hiyo amefariki, amefukuzwa, ameacha kazi, amepandishwa cheo, amepewa wadhifa mwingine au iwapo nafasi itakuwa tupu kwa sababu nyingine yoyote inayo kubalika.

   b. Iwapo nafasi mpya itakuwa imeundwa na Halmashauri Kuu Taifa.

7. Mtumishi aliyepandishwa cheo lazima atoe taarifa ya maandishi ya kukubali ama kukataa dhamana aliyokabidhiwa katika muda usiozidi mwezi mmoja baada ya kupata taarifa ya kupandishwa cheo.

8. Upandishwaji wa cheo utakuwa umekamilika pale ambapo aliyepandishwa cheo atakuwa amekubali dhamana alizopewa kwa mujibu wa kijifungu (7) cha kifungu hiki.

9. Itakuwa ni moja kati ya masharti ya kupandishwa cheo kwamba mwenye kupandishwa cheo awe katika majaribio ya cheo chake kipya kwa muda wa miezi sita .

10. Endapo baada ya kumalizika miezi sita mwenye kupandishwa cheo ataonekana si mwenye kuyamudu madaraka yake mapya na kama hakutakuwa na uamuzi wowote mwingine, anaweza akarudishwa katika cheo chake alichokuwa nacho kabla ya kupandishwa cheo alicho nacho sasa.

11. Uamuzi unaohusiana na hatua za kuchukuliwa iwapo mwenye kupandishwa cheo ameshindwa kumudu dhamana zake mpya kufuatana na kijifungu(10) cha kifungu hicho ufanywe na yule aliyempandisha cheo.

12. Mtumishi wa Chama ataweza kufanya kazi kwa kuazimwa kwa muda katika Utumishi wa Serikali ya Muungano au ya Zanzibar na kupata idhini ya Halmashauri Kuu ya Taifa.

13. Mtumishi wa kuazimwa atafanya kazi katika sehemu alizoazimwa kwa muda wa miaka miwili. Kipindi hicho kinaweza kuongezwa kwa miaka miwili mingine ambapo baada ya kumalizika muda huo wa vipindi viwili vya miaka miwili kila kimoja, mtumishi anayehusika atalazimika kuchagua kubaki kuwa mtumishi wa kudumu katika sehemu alikoazimwa au kurudi katika sehemu aliyotoka ila pale chombo kilicho muazima kitakapoomba kwa **Katibu Mkuu** na kukubalika kuwa mfanya kazi huyo aendelee tena.

14. Muda aliotumikia mfanyakazi kwa njia ya kuazimwa utahesabika katika sehemu anayo tumikia. Endapo mfanyakazi wa kuazimwa atapendelea kuhamishwa moja kwa moja katika sehemu aliyoazimwa baada ya muda kumalizika atalazimika kujiuzulu katika sehemu ya chama anayotoka na anaweza kupewa tunzo ya kazi yake.

15. Mtumishi wa kuazimwa atakuwa na haki ya kupandishwa cheo, kupata nyongeza ya mshahara pamoja na kupata haki nyinginezo zote za Chama zinazoambatana na masharati katika sehemu ya Chama aliyoazimwa.

16. Kutakuwa na ripoti za **Siri** kwa ajili ya kila mtumishi zitakazotayarishwa na Katibu Mkuu au Mkuu wa Idara kila mwaka kwa mpango ufuatao:-

a. Sehemu ya pili ijazwe na Katibu Mkuu na kuwekwa katika ofisi vizuri.

b. Ripoti ya mwendo mzuri au mbaya ya watumishi lazima iambatane na barua ya kumpongeza au ya Onyo alilopewa kwa kadri itakavyokuwa mfanyakazi anayehusika kutoka kwa Mkurugenzi wake.

17. Ikiwa mtumishi anayeondoka katika sehemu yake ya kazi kwa likizo ama safari au kama atakuwa amepewa uhamisho kwenda sehemu nyingine na iwapo kuondoka kwake kutakuwa katika kipindi ambacho ripoti yake ya Siri inahitajika, Mkuu wake wa kazi atatakiwa aitayarishe na kuikamilisha ripoti hiyo kabla ya mfanyakazi huyo hajaondoka katika sehemu yake aliyoko. Iwapo ripoti inayohusika inamhusu mtumishi aliyehamishwa, ripoti hiyo italazimu ipelekwe katika shemu aliyohamishiwa ikiwa ni nje ya Chama.

18. Iwapo mtumishi amepatiwa uhamisho wa ndani ya Chama kumbukumbu zake zote za kawaida zitachukuliwa kama watumishi waliohamishwa sehemu moja ndani ya chama. Taarifa za siri zitabaki katika ofisi ya Katibu Mkuu tu.

## MAPATO NA UDHIBITI WA MALI YA CHAMA.

1. Chama kitakuwa na njia ya kujipatia fedha za matumizi na mali kwa njia zifuatazo:-
   a. Michango ya uanachama.
   b. Ruzuku kutoka kwa wanachama, Wafadhili na Wahisani wa ndani na nje ya nchi na ruzuku kutoka Serikalini.

2. Chama kitajipatia mapato kutokana na .

   a. Shughuli maalum za Kijamii, Tafrija na Burudani na njia nyingine zozote zitakazokubaliwa na Halmashauri Kuu.
   b. Mapato kutoka miradi mbali mbali ya uchumi kama vile viwanda, mashirika na makampuni.

3. Watia sahihi wa hundi za Chama wateuliwe na Halmashauri Kuu Taifa kwa hundi za Makao Makuu watateuliwa na Kamati ya Utendaji Taifa.

4. Shughuli zote za mapato, Mali fedha, Madai na Madeni ya chama zitasimamiwa na Bodi ya Wadhamini kulingana na utaratibu wa sheria ya Vyama vya Siasa au sheria nyingine yeyote iliyotungwa na Bunge la Jamuhuri ya Muungano au Baraza la wakilishi.

## UWEKAJI MZURI WA MALI ZA CHAMA

1. Mweka Hazina wa Chama atawajibika kuweka madaftari ya mali na vitabu vya fedha kwa mujibu wa sheria za Nchi.

2. Mali isiyoondosheka ya Chama itaorodheshwa na kuhifadhiwa ndani ya *MADAFTARI YA CHAMA* (Register Book).

3. Mapato na matumizi ya fedha ya Chama yatafanywa kwa mujibu wa kanuni za fedha. Malipo yatafanywa kwa stakabadhi ambazo zitatolewa kwa idhini ya Halmasahuri Kuu Taifa.

4. Ukaguzi wa mali na fedha za Chama utafanywa na kampuni au makampuni yaliosajiliwa Nchini kwa mujibu wa sheria za Nchi na kanuni za Chama baada ya kukubaliwa na Halmashauri Kuu Taifa.

5. Mali zote za Chama zinazoondosheka zitahifadhiwa na Mhakiki Mali wa chama chini ya Katibu Mkuu.

6. Chama kitakuwa na kanuni ndogo ndogo za kudhibiti matumizi ya fedha kila siku chini ya idara ndogo ya UDHIBITI WA NDANI wa fedha, **(Internal Audit)**.

7. Fedha za chama zitawekwa katika Benki ambayo itakubaliwa au ambazo zitakubaliwa na Kamati Utendaji ya Taifa.

## BODI YA WADHAMINI.

1. Bodi itakutana mara mbili kwa mwaka.

2. Bodi itateua Mwenyekiti na Katibu wake.

3. Katibu wa Bodi ataweka vizuri kumbukumbu za vikao, Madaftari ya mali za Chama na maagizo yake kwa Chama.

## VITENGO VYA CHAMA.

1. Chini ya ibara ya 8(c) na (d) na (e) (i-x) ya Katiba ya Chama, Halmashauri Kuu Taifa ina uwezo wa kuunda, kufuta au kuongeza vitengo vya Chama katika ngazi ya Taifa ikiwa ni pamoja na kuviunaganisha au kuvitenganisha pale inapohitajika, kama ambavyo inahisi inafaa ili kusaidia utekelezaji mzuri wa Sera pamoja na shughuli nyingine za Chama.

2. Kwa kutumia mamlaka yalioelezwa katika kifungu cha (c) cha ibara hiyo Halmashauri Kuu Taifa linaanzisha vitengo zifuatazo:-

   a. Kitengo cha Ulinzi na Usalama.
   b. Kitengo cha Fedha,Uchumi na mipango.
   c. Kitengo cha Wanawake.
   d. Kitengo cha Vijana.
   e. Kitengo cha Sera za Mambo ya Nje na Uhusiano kimataifa.

## WAKURUGENZI WA CHAMA.

1. Kutakuwa na Wakurugenzi na Naibu Wakurugenzi ambao watakua viongozi na watendaji wakuu wa Vitengo vya chama Vilivyoanzishwa na Halmashauri Kuu Taifa kwa mujibu wa kanuni hizi.

2. Kazi ya Mkurugenzi na Naibu Mkurugenzi ni kutekeleza kwa ufanisi mkubwa majukumu ya Kitengo anachokiongoza kama yalivyoelezwa katika kanuni hizo au / na maelekezo ya Halmashauri Kuu Taifa.

3. Mwenyekiti au Katibu Mkuu anaweza kumtuma Mkurugenzi yoyote kufanya kazi maalum kwa muda maalum nje ya shughuli za Idara yake kwa manufaa ya Chama.

## MAJUKUMU YA VITENGO VYA CHAMA.

Kila Kitengo kitakuwa na kazi na majukumu kama yalivyoelezwa katika kanuni hizi lakini Halmashauri Kuu Taifa pia inaweza kuongeza au kupunguza kazi na madaraka hayo kwa kadri itakavyoona inafaa.

## KITENGO CHA ULINZI NA USALAMA.

Mkurugenzi wa kitengo cha Ulinzi na Usalama atafanya kazi chini ya **Mratibu Uhamasishaji Taifa** na kazi zake ni kama ifuatavyo:-

1. Atahakikisha Ulinzi na usalama wa Viongozi Wakuu Chama.

2. Atahakikisha Ulinzi na Usalama unakuwepo katika Mikutano yote inayoandaliwa na chama.

3. Atahakikisha kunakuwa na ulinzi wa Mali na vitega uchumi vya Chama na atafanya kazi zake kadri atakavyopangiwa na Mratibu Uhamasishaji Taifa.

## KITENGO CHA FEDHA , UCHUMI NA MIPANGO.

Mkurugenzi wa kitengo cha Fedha, Uchumi na Mipango atafanya kazi chini ya **Mweka Hazina wa Chama Taifa** na atakuwa na majukumu yafuatayo:-

1. Atatunza mali na fedha za Chama.

2. Atakuwa mfano bora wa utendaji na uaminifu katika jamii nzima ya Tanzania.

3. Atahakikisha utunzaji bora wa mahesabu ya Chama na kutayarisha kwa ajili ya ukaguzi.

4. Atakuwa na wajibu wa kukishauri Chama juu ya upatikanaji na usimamizi wa mali kwa ushirikiano na Wadhamini wa Chama.

5. Atahakikisha usalama wa mali na biashara za chama zilizo mikononi mwa Bodi ya wadhamini wa Chama, na atahakikisha kuwa ukaguzi wa mali na mahesabu ya fedha unafanyika ipasavyo.

6. Atashirikiana na vyombo vingine vya fedha ndani na nje ya Nchi , kwa manufaa ya Chama.

7. Atatayarisha mafunzo ya udhibiti na usimamizi wa fedha kwa watumishi wa chama ili wawe na ujuzi wa uhakika na kuweza kuhakikisha fedha na mali ya Chama zinakuwa salama.

8. Atafanya utafiti wa kina juu ya mbinu za utekelezaji mzuri wa itikadi ya utajirisho.

9. Atabuni na kusimamia miradi ya kiuchumi ya chama na utekelezaji wa miradi yao.

10. Atakifanya Chama kujitegemea wakati wote.

## KITENGO CHA WANAWAKE.

Mkurugenzi wa kitengo cha Wanawake atafanya kazi chini ya Mratibu wa Wanawake Taifa na atakua na majukumu yafuatayo:-

1. Atasaidia kuondoa hali kutojiamini inayosababishwa na mila za jadi na fikra potofu kuhusu jinsia yao.

2. Atawakusanya wanawake katika jumuia mbali mbali za utendaji, kwa lengo la kufikiria, kuamua, kupanga, kubuni na kutekeleza uzalishaji, na ugawaji mali, bidhaa na huduma kwa njia ya utajirisho kwa lengo la kuinua hali ya maisha ya kila mwanamke na kwa njia hiyo kuwafanya wawe wachangiaji wakubwa wa pato la taifa.

3. Atasaidia kuwapatia elimu na mafunzo wanawake ili kuwawezesha kujitegemea katika kufikiria, kuamua kupanga, kubuni na kutekeleza uzalishaji.

4. Atawashirikisha wanawake katika kusimamia na kuzilinda wakati wote haki za binadamu na haki za watu, pamoja na kuwaheshimu, kuwasaidia wazee na wasiojiweza popote walipo ndani ya Nchi.

5. Atawaongoza Wanawake wabuni miradi ya uchumi ili wainue hali zao za maisha na pia waweze kuchangia katika mfuko wa Taifa.

6. Atashirikian na Taasisi za kisheria na haki za binaadamu ili kuhakisha kwamba Wanawake katika shughuli zao hawabugudhiwi au kudhalilishwa kwa sababu ya jinsia.

7. Atapanga kuwapatia elimu akina Mama kwa njia ya Semina, warsha, kozi fupi na kadhalika kwa kushirikiana pamoja na vikundi au mashirika ya kimataifa yanayo shughulikia masuala ya maendeleo ya Wanawake na Watoto.

8. Atashirikiana na vikundi vya uzalishaji vya wanawake kitaifa na kimataifa ili kupanua mwamko na maslahi ya wanawake.

9. Atatetea haki za watoto na kuhakikisha wanapata malezi bora na elimu yenye manufaa.

10. Atahakikisha kuwapatia elimu kina mama kwa njia ya Mikutano, Semina, Warsha na Makongamano ya kupambana na majanga ya Kitaifa kitaifa kama UKIMWI na kadhalika

## KITENGO CHA VIJANA.

Kijana katika UMD ni Mwanachama yoyote wa kike au wa kiume mwenye umri usiozidi miaka thelathini na tisa (39)

Mkurugenzi wa kitengo cha Vijana atafanya kazi chini ya **Mratibu Vijana Taifa** na atakuwa na kazi majukumu kama ifuatavyo:-

1. Atabadili dhana ya kuwachukulia vijana kuwa ndio viongozi wa kesho na kuwaandaa kuwa viongozi wa leo. Na kuwaepusha vijana kuwa kundi la ukandamizwaji tu. Atahakikisha kuwa vijana wanahusishwa katika hatua zote za uamuzi, upangaji, ubunifu na utekelezaji katika shughuli za kuichumi na za kijamii.

2. Atatilia maanani kwamba, Vijana ndio watekelezaji wakuu wa shughuli zote za kitaifa, bila kusahau kwamba wao ndio chemchemu ya viongozi

na ndio nguvu kazi na askari wa mstari wa mbele kuliokoa taifa na majanga, vita na uvamizi.

3. Atawakusanya Vijana katika Jumuia mbali mbali za utendaji, kwa lengo la kufikiria kuamua, kupanga, kubuni na kutekeleza uzalishaji na ugawaji mali, bidhaa na huduma kwa njia ya utajirisho kwa lengo la kuinua hali ya maisha ya kila kijana, na kwa njia hiyo kuwafanya wawe wachangiaji wakubwa wa pato la Taifa

4. Atawasaidia Kuwapatia vijana elimu na mafunzo ili waweze kujitegemea katika kufikiria kuamua, kupanga, kubuni na kutekeleza uzalishaji.

5. Atawasaidia vijana kupata elimu ya juu na kufuatilia utoaji elimu nchini na kushirikiana na vyombo vya Serikali na vya Kijamii katika kuhakikisha viwango vya elimu vinapanda.

6. Ataimarisha juhudi za vijana katika harakati za Ujenzi wa Taifa la karne ya ishirini na moja.

7. Atafufua na kuimarisha historia na Utamaduni wa kweli wa Taifa letu kwa kuwashirikisha Vijana na kuwalea ili wathamini wanakotoka,. desturi na mila ambazo ni za Maendeleo na haziendi kinyume na Haki za binaadamu.

8. Atawashirikisha Vijana katika kusimamia na kuzilinda wakati wote haki za Binaadamu pamoja na kuwaheshimu, kuwasaidia wazee na wasiojiweza popote walipo ndani ya nchi.

9. Atawahamasisha vijana ili wawe ndio askari wa mstari wa mbele wa Taifa katika kukabili na kupambana na maafa yanayotokea, kutokana na majanga hasa janga la **UKIMWI.**

10. Atajenga uhusiano mzuri na vyombo vya Fedha vya nchi na Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali ili kusaidia juhudi za Maendeleo halali.

## KITENGO CHA MAMBO YA NJE NA UHUSIANO WA KIMATAIFA.

Mkurugenzi wa kitengo cha Mambo ya Nje na Uhusiano wa Kimataifa atakuwa chini ya Katibu Mkuu na atafanya kazi zifuatazo:-

1. Atajenga uhusiano Mwema kati ya Chama na Vyama vingine vya Kisisasa vilivyo na mtazamo sawa na chama chetu hapa nchini, Afrika na ulimwengu kwa jumla.

2. Atasimamia maandalizi ya safari za Viongozi wa Chama kwenda nchi za nje na kupokea wageni wa Chama kutoka vyama rafiki au kutokea nchi za nje.

3. Atajenga uhusiano wa karibu na nchi za nje ili kupata uelewano mzuri na nchi hizo.

4. Atazingatia Sera za Chama ili zieleweke na Vyama rafiki duniani

5. Ataratibu misaada yoyote ya hali na mali kutoka vyama rafiki vya nje ya nchi.

6. Atafuatilia kwa karibu Shughuli za Watanzania walioko Nchi za nje ili kuhakikisha kwamba wananchi wote wanashughulikiwa matatizo yao ipasavyo na wanatendewa haki huko waliko, na wao wanaheshimu sheria za nchi wanamoishi kwa nia ya kulinda heshima ya Tanzania.